# MAJIRA YA JOTO 2025

Kipindi cha 1: Juni 9 – Juni 27 | Kipindi cha 2: Juni 30 – Julai 23

YOUTHCITY

## *WITO*

YouthCity huendeleza maendeleo chanya ya vijana katika Jiji la Salt Lake kwa kuwapa fursa za nje ya shule kwa ajili ya maendeleo ya kijamii, kihisia, kiujuzi, kitabia na kiuraia katika mazingira jumuishi

## *MADARASA*

Madarasa yanategemeana na anachopenda mwanafunzi na hubadilika kila kipindi. Mifano baadhi inahusisha:

Kuteleza kwa vibao
Kutengeneza Filamu
Kubuni Mchezo wa Video
Kupika
Muziki
Uchunguzi wa Kompyuta
Kufanya Podikasti
Safari za Nje
Sanaa za Kuona
Kutengeneza
Kitabu
STEM
Kuchunguza Jiji Tabia za Kiafya
Uandishi wa Kibunif

## *GHARAMA ZA PROGRAMU*

$15 - $578 kwa kipindi* Kuondolewa kwa ada na ufadhili wa masomo kwa wakimbizi vinapatikana.
*kutegemeana na kipato na ukubwa wa familia.










## *MAENEO*

***CENTRAL CITY***
615 S 300 E
ERICA ANDINO
801-381-6836

***FAIRMONT PARK***
1040 E 2250 S
LAUREN UNDERWOOD
801-573-6519 | 801-466-0904

***LIBERTY PARK***
1031 S 600 E
JESS UNG
801-558-8223 | 801-533-0485

***OTTINGER HALL***
233 N CANYON RD
CONNIE PAREDES-POZAS
801-573-1349 | 801-320-0939

***SORENSON UNITY CENTER***
***DARASA LA 3 - 6***
1383 S 900 W
LOLA PAREDES
801-879-9678 | 801-535-6532

***SORENSON MULTI-CULTURAL CENTER***
***DARASA LA AWALI - LA 2*** 855 W CALIFORNIA AVE
FERNANDO PUGA
385-282-9933

***FAIRPARK***
855 W CALIFORNIA AVE
ANGEL GOMEZ
385-495-8960

Programu za majira ya joto kwa vijana darasa la awali – darasa la 6
Kwa taarifa zaidi tembelea: youthcity.com | Jumatatu - Ijumaa 2:30 asubuhi - 11:30 jioni

# MSAMAHA WA ADA MSIMU WA KIANGAZI 2025

YOUTHCITY

Kipindi cha 1: Juni 9 – Juni 27 | Kipindi cha 2: Juni 30 – Julai 23

Ada, kama ilivyobainishwa na Ushirika wa Jiji la Salt Lake, zitaondolewa kulingana na viwango vya Idara ya Huduma za Kazi kwa wanafunzi ambao wazazi au walezi wao halali wamethibitisha ushahidi wa kutokuweza kulipa. Wasioweza kulipa wanaelezewa kuwa kama ni wale walio katika kifungo cha kiserikali, huduma ya malezi, au wanaopokea usaidizi wa umma katika namna ya Msaada kwa Watoto Tegemezi, Kipato cha Nyongeza cha Kujitunza, au wanastahiki kulingana na Miongozo ya Stahiki ya Kipato ya Julai 1, 2024 hadi Juni 30, 2025; na, kwamba maamuzi ya kesi kwa kesi yanafanyika kwa wale ambao hawakidhi chini ya moja ya viwango vilivyobainishwa, lakini ambao, kwa sababu ya mazingira yasiyowezeshi kama vile, lakini yasiyoishia tu, mizigo isiyo ya kawaida ya kifedha kama vile kupoteza au punguzo la kipato kilichokuwa imara au matumizi ya kimatibabu yasiyo ya kawaida, kimsingi hawataweza kulipa ada. (Risiti ya fidia ya kutokuajiriwa na/au chakula cha mchana cha shule kilichopunguzwa gharama haihusishi msaada wa umma kama ilivyoelezewa hapo juu.)

---

- Ikiwa mtoto wako anakidhi kupata chakula cha mchana cha bure kwenye shule yoyote iliyosajiliwa na Bodi ya Elimu ya Jimbo la Utah, basi ada zote za programu ya YouthCity zinaweza kuondoleewa.

- Ikiwa ombi la kuondolewa ada limekataliwa, mwanafunzi au mzazi anaweza kukata rufaa juu ya uamuzi huo kwa Ushirika wa Jiji la Salt Lake.

- Taarifa zote kwenye ombi hili zitatunzwa kwa usiri

JINA LA MSHIRIKI: ____________________ DARASA: __________

ANWANI: ____________________ MJI: __________ ZIP: __________

SHULE: ____________________ WILAYA: ____________________

JINA LA MZAZI/MLEZI: ____________________ SIMU YA MZAZI/MLEZI: __________

**ENEO (tiki moja):**

☐ Central City ☐ Fairmont Park ☐ Ottinger Hall ☐ Liberty Park ☐ Fairpark

☐ Sorenson Multi-Cultural Center Darasa la awali-la 2 ☐ Sorenson Unity Center Darasa la 3-la 6

**Ninathibitisha (ninaahidi) kwamba taarifa zote kwenye ombi hili ni kweli na kwamba kipato chote kimeripotiwa. Ninaelewa kwamba viongozi wa jiji wanaweza kuthibitisha (kuchunguza) taarifa hizi. Ninaelewa kwamba ikiwa ninatoa taarifa za uongo kwa kusudi, ninaweza nikashitakiwa.**

____________________ TAREHE: ____/____/____

siku/mwezi/mwaka

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Imethibitishwa:

# MAJIRA YA JOTO 2025

FOMU YA USAJILI

YOUTHCITY

Kipindi cha 1: Juni 9 – Juni 27 | Kipindi cha 2: Juni 30 – Julai 23

MSHIRIKI

JINA: ______________________ KUZALIWA: ____/____/____ UMRI: ____ JINSIA: ______
siku/mwezi/mwaka

ANWANI: ______________________ JINA LA MZAZI: ______________________

MJI: ______________________ ZIP: __________ #INAYOPATIKANA: ____-____-____ # YA SMS: ____-____-____

BARUA PEPE YA KWANZA: ______________________ BARUA PEPE MBADALA: ______________________

SHULE: ______________________ DARASA: ____ ID YA MWANAFUNZI/#YA CHAKULA CHA MCHANA: ______

ASILI:

- ☐ ASIA
- ☐ MWEUSI/MWAFRIKA
- ☐ MUHINDI-MZUNGU/MZUNGU
- ☐ MKAZI WA PASIFIKI
- ☐ MZAWA WA MAREKANI
- ☐ NYINGINE

KABILA:

- ☐ MUHISPANIA AU MLATINO
- ☐ ASIYE MUHISPANIC AU MLATINO

**Mzazi au Mlezi Halali ni lazima asome na kusaini chini kwa ajili ya mtoto kushiriki katika YouthCity**

**Msamaha & Fidia:** Ninatambua na kukubali kwamba ushiriki wa mtoto wangu katika shughuli hizi unaweza kuhusisha kuumia kimwili na/au kuumia kihisia kwangu mwenyewe na/au mtoto. Kwa kuzingatia kwa mtoto wangu kuruhusiwa kushiriki katika matukio kama hayo, kwa niaba yangu, mtoto wangu, warithi wangu, wasimamizi wangu wa mirathi na watawala, kwa hiari na kwa kujuwa ninasamehe uzembe juu ya jeraha lolote ambalo linaweza kutokana na ushiriki wa mtoto, isipokuwa lile lililosababishwa na uongozi mbaya wa kukusudia wa wafanyakazi wa YouthCity.

**Marejesho ya fedha:** YouthCity inaweza kushikilia 25% ya rejesho la fedha (ada ya usajili kwenye programu) kwa ajili ya gharama za kiutawala. Marejesho yote ya fedha yanaweza kuombwa kibinafsi, yakiambatana na ombi la rejesho la fedha kimaandishi. Hakuna marejesho ya pesa yatakayotolewa baada ya siku ya kwanza ya programu.

**Makusanyo:** Ninakubali kuilipa Ofisi ya Mwanasheria wa Jiji la Salt Lake kwa ajili ya makusanyo. Ninaelewa kwamba uchelewashwaji wowote wa malipo kwa siku 30 au zaidi utakabidhiwa kwa Ofisi ya Mwanasheria wa Jiji la Salt Lake kwa ajili ya makusanyo.

**Matibabu ya Dharura:** Ninatoa idhini kwa wafanyakazi wa programu ya Jiji la Salt Lake kutenda kwa niaba yangu kulingana na busara zao katika mazingira ya dharura inayomhusisha mtoto wangu, na kukubali kuchukua wajibu wote kwa ajili ya gharama zote, za kimatibabu au vinginevyo, ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na hilo. Ninaelewa kwamba mimi au kampuni yangu ya bima itatakiwa kulipa gharama kwa ajili ya matibabu ya dharura kama hayo.

**Ruhusa ya Usafiri:**
Ninatoa ruhusa yangu kwa watumishi wa YouthCity kumsafirisha mtoto wangu au kumlinda kwa ajili ya safari za kwenda maeneo ya kujifunza. Ninakubali na kwa hiari ninakabidhi hatari yote, ambayo inaweza kuhusiana na au kutokana na kusafiri kwa mtoto wangu au ulinzi wa usafiri kwa Programu ya YouthCity. Zaidi ninakubali kuwaachia huru Wilaya ilipo Shule ya Jiji la Salt Lake, YouthCity, Ushirika wa Jiji la Salt Lake na Mkoa wa Salt Lake, mawakala wake, idara, maafisa, wafanyakazi wa mawakala na wafadhili wote na/au viongozi na wafanyakazi wa chombo au mtu yeyote tajwa, wawakilishi wao, washirika wa mawakala, wakurugenzi, watumishi, wanaojitolea na wafanyakazi dhidi ya deni, madai, matakwa, vitendo na sababu za vitendo vyovyote au vyote kwa hasara, madai, uharibifu, majeraha, ugonjwa, gharama za mwanasheria, au dhara la aina au asili yeyote kwangu au kwa mtoto wangu au mlezi linalotokana na shughuli yoyote au yote inayohusiana na shughuli zilizotajwa awali. Nimesoma kwa uangalifu na kuelewa maudhui ya fomu hii kuhusu usafirishwaji wa mtoto wangu au mlezi.

**Ruhusa ya Kupiga Picha:** Ninatoa ruhusa ya kupigwa picha na kurekodiwa video kwa mtoto wangu wa kiume/kike anavyoshiriki katika shughuli za Jiji la Salt Lake na vitumike katika nyenzo za matangazo kwa programu hii au programu nyingine za washirika. Ninaelewa kwamba picha na/au video hizi zinaweza kutumika katika brosha, programu za video zilizohaririwa, mtandaoni na vitu vingine vya matangazo kwa ajili ya kuzitaarifu pande zinazovutiwa kuhusu shughuli za Jiji la Salt Lake.

**Fursa Sawa:** Ushirika wa Salt Lake YouthCity unatoa fursa sawa kwa washiriki bila ya kujali asili, imani, jinsia au uwezo wa kulipa na kufuatia ombi utatoa malazi stahiki kwa watu wenye ulemavu.

**Tamko la kutokubagua:** Kulingana na sheria ya haki za raia ya Serikali ya Shirikisho na Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA) kanuni za haki za raia na sera, USDA, mawakala wake, ofisi, na wafanyakazi, na taasisi zinazoshiriki katika au zinazosimamia programu za USDA zinazuiwa kubagua kulingana na asili, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, imani ya kidini, ulemavu, umri, imani za kisiasa, au kulipiza kisasi au ulipizaji kisasi kwa shughuli ya awali ya haki za kiraia katika programu yoyote au shughuli inayoendeshwa au kufadhiliwa na USDA. Watu wenye ulemavu ambao wanahitaji njia mbadala za mawasiliano kwa ajili ya taarifa za programu (m.f. Breli, chapisho kubwa, mkanda wa sauti, Lugha ya Ishara ya Kimarekani, n.k.), wanapaswa kuwasiliana na Wakala (wa Jimbo au Mtaa) ambapo walituma maombi kwa ajili ya fidia. Watu ambao ni mabubu, wenye ugumu kusikia au wenye ulemavu wa kuongea wanaweza kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya Rilei ya Serikali ya Shirikisho kwenye namba (800) 877-8339. Kwa nyongeza, taarifa za programu zinaweza zikapatikana katika lugha nyingine zaidi ya Kiingereza. Ili kuwasilisha lalamiko la ubaguzi unaohusu programu, kamilisha Fomu ya Programu ya USDA ya Lalamiko la Ubaguzi, (AD-3027) inayopatikana mtandaoni kwenye: http://www.ascr.usda.gov/complaint_filing_cust.html, na kwenye ofisi yoyote ya USDA, au andika barua ukiielekeza USDA na toa katika barua hiyo taarifa zote zilizoombwa katika fomu. Ili kuomba nakala ya fomu ya malalamiko, piga simu namba (866) 632-9992. Wasilisha fomu au barua yako kamili USDA kwa: (1) barua pepe: Idara ya Kilimo ya Marekani Ofisi ya Katibu Msaidizi anayeshughulikia Haki za Kiraia 1400 Independence Avenue, SW Washington, D.C. 20250-9410; (2) faksi: (202) 690-7442; or (3) barua pepe: program.intake@usda.gov. Taasisi hii hutoa fursa kwa usawa.

**Kwa kusaini nyaraka hii, ninakubali kwamba nimesoma maudhui na uwazi wake, na ninayakubali masharti yake.**

SAINI YA MZAZI: ______________________ TAREHE: ____/____/____
siku/mwezi/mwaka

**ENEO (tiki moja):** ☐ Central City ☐ Fairmont Park ☐ Ottinger Hall ☐ Fairpark

☐ Liberty Park ☐ Sorenson Multi-Cultural Center Darasa la awali-la 2 ☐ Sorenson Unity Center Darasa la 3-la 6

**GHARAMA:** Ada hutofautiana kutoka $15 hadi $578 kwa mwanafunzi, kwa mwezi kwa ajili ya wakazi wa Jiji la Salt Lake, kulingana na ukubwa wa familia na kipato. Gharama zinaweza kulipwa mtandaoni kwa credit card au debit card au moja kwa moja kwa hundi au oda ya pesa.

Tafadhali kamilisha fomu iliyo hapa chini ili kufahamu ada yako.

Ukubwa wa familia: ☐ Jumla ya kipato cha familia kwa mwaka (kabla ya makato): ☐

☐ **A** – Jumla ya kipato cha familia yetu kwa mwaka ni ***zaidi*** ya kilichoorodheshwa hapa chini.
Tunastahili gharama ya: **Kipindi cha 1: $578 Kipindi cha 2: $578**

| Ukubwa wa familia | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipato | $73,950 | $83,200 | $92,400 | $99,800 | $107,200 | $114,600 | $122,000 |

☐ **B** - Jumla ya kipato cha familia yetu kwa mwaka ni ***kidogo*** kuliko au sawa na kilichoorodheshwa hapa chini.
Tunastahili ada ya: **Kipindi cha 1: $331 Kipindi cha 2: $331**

| Ukubwa wa familia | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipato | $73,950 | $83,200 | $92,400 | $99,800 | $107,200 | $114,600 | $122,000 |

☐ **C** - Jumla ya kipato cha familia yetu kwa mwaka ni ***kidogo*** kuliko au sawa na kilichoorodheshwa hapa chini.
Tunastahili ada ya: **Kipindi cha 1: $221 Kipindi cha 2: $221**

| Ukubwa wa familia | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipato | $55,400 | $62,400 | $69,300 | $74,880 | $80,400 | $85,980 | $91,500 |

☐ **D** - Jumla ya kipato cha familia yetu kwa mwaka ni ***kidogo*** kuliko au sawa na kilichoorodheshwa hapa chini.
Tunastahili ada ya: **Kipindi cha 1: $147 Kipindi cha 2: $147**

| Ukubwa wa familia | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipato | $46,200 | $52,000 | $57,750 | $62,400 | $67,000 | $71,650 | $76,250 |

☐ **E** - Jumla ya kipato cha familia yetu kwa mwaka ni ***kidogo*** kuliko au sawa na kilichoorodheshwa hapa chini.
Tunastahili ada ya: **Kipindi cha 1: $74 Kipindi cha 2: $74**

| Ukubwa wa familia | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipato | $27,750 | $31,200 | $34,650 | $37,450 | $40,200 | $43,000 | $45,750 |

☐ **F** - Jumla ya kipato cha familia yetu kwa mwaka ni ***kidogo*** kuliko $10,000 (ukubwa wowote wa familia) We
Tunastahili ada ya: **Kipindi cha 1: $15 Kipindi cha 2: $15**

☐ **G** – Mtoto wangu anakidhi kupata chakula cha mchana bila malipo na hivyo ninaomba kuondolewa ada. Tafadhali wasiliana na Meneja wa Programu za Kijamii kwa ajili ya fomu ya kuondolewa ada.

☐ **H** – Mtoto wangu alikuja Marekani kama mkimbizi. Ninaomba ufadhili kamili wa masomo.

☐ **Nitafanya malipo yajayo mtandaoni** ☐ **Nitafanya malipo yajayo kwa hundi au oda ya pesa**

**Ninathibitisha (ninaahidi) kwamba taarifa zote kwenye ombi hili ni kweli na kwamba kipato chote kimeripotiwa. Ninaelewa kwamba viongozi wa jiji wanaweza kuthibitisha (kuchunguza) taarifa hizi. Ninaelewa kwamba ikiwa ninatoa taarifa za uongo kwa kusudi, ninaweza nikashitakiwa.**

JINA LA MTOTO: ______________________ JINA LA MZAZI: ______________________

SAINI YA MZAZI: ______________________ TAREHE: ____/____/____
siku/mwezi/mwaka

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Imethibitishwa:

## TAARIFA ZA MAWASILIANO WAKATI WA KUONDOKA NA DHARURA MAJIRA YA JOTO 2025

**#1 MZAZI/MLEZI:**__________ UHUSIANO: __________ NAMBA: ___-___-___

BARUA PEPE: __________ TUMA TAARIFA ZA PROGRAMU: NDIO ☐ HAPANA ☐ KWA:BARUA PEPE ☐ SMS ☐

**#2 MZAZI/MLEZI:**__________ UHUSIANO: __________ NAMBA: ___-___-___

BARUA PEPE: __________ TUMA TAARIFA ZA PROGRAMU: NDIO ☐ HAPANA ☐ KWA:BARUA PEPE ☐ SMS ☐

**MZAZI/MLEZI MBADALA:**__________ UHUSIANO: __________ NAMBA: ___-___-___

BARUA PEPE: __________ TUMA TAARIFA ZA PROGRAMU: NDIO ☐ HAPANA ☐ KWA:BARUA PEPE ☐ SMS ☐

**MACHAGUO YA KUONDOKA:** TAFADHALI TIKI YOTE YANAYOHUSIKA

☐ Mzazi/Mlezi atamchukuwa mtoto saa 11:30 jioni

☐ Mtoto anaweza kuondoka mwenyewe na kwenda nyumbani

☐ Mtoto anaweza kuondoka mwenyewe na kwenda nyumbani na kaka yake mkubwa au

JINA LA NDUGU: __________ NAMBA YA SIMU:__________

JINA LA NDUGU: __________ NAMBA YA SIMU:__________

☐ Mtu mzima mwingine (wengine) anayeweza kumchukuwa mtoto

JINA:__________ NAMBA YA SIMU:__________

JINA:__________ NAMBA YA SIMU:__________

**MTOTO ANA MIZIO:** **NDIO** ☐ **HAPANA** ☐ TAFADHALI ORODHESHA:__________

**MTOTO ANA MAHITAJI MAALUM:** **NDIO** ☐ **HAPANA** ☐ TAFADHALI ORODHESHA:__________

**TAARIFA KUHUSU KUOGELEA:** ☐ Mtoto wangu anaweza kuogelea ☐ Mtoto wangu hafahamu jinsi ya kuogelea

**KATIKA KESI YA DHARURA:** TAFADHALI ORODHESHA WALAU WATU WAWILI WA KUWASILIANA NAO

JINA: __________ NAMBA YA SIMU: __________

JINA: __________ NAMBA YA SIMU: __________

JINA: __________ NAMBA YA SIMU: __________

**Katika kesi ambapo mtoto wangu ameumia, ninatoa ruhusa ya mtoto wangu kutibiwa na mtoa huduma mwenye vigezo katika kituo chochote halali cha afya**

SAINI YA MZAZI: __________ TAREHE: ___/___/___
siku/mwezi/mwaka

## SERA YA MALALAMIKO YA PROGRAMU YA BAADA YA SHULE NA MAJIRA YA JOTO YA YOUTHCITY

Kama mshiriki wa programu, mzazi, au mlezi ana tatizo na programu au mfanyakazi wa programu ya baada ya shule na majira ya joto ya YouthCity, utaratibu ufuatao wa malalamiko unapaswa kutumiwa.

Ikiwa ni sawa, tafadhali jadili tatizo hilo na Meneja Mkuu wa Programu ya Jamii au Msaidizi wa Programu kwanza.

Ikiwa hauwezi kujadili tatizo hilo na uongozi wako wa programu kwa eneo husika, au hauwezi kufikia suluhisho, tafadhali wasilisha tatizo lako kwa maneno ya mdomo au katika maandishi kwa Mkurugenzi Mshirika wa Vijana na Familia. Mkurugenzi Mshirika atawasiliana na wewe kujadili matatizo hayo na wewe pamoja na wafanyakazi wanaohusika kupata suluhisho.

Ikiwa tatizo lako halijasuluhishwa kukuridhisha, au kama una tatizo kumhusu Mkurugenzi Mshirika wa programu, unaweza kuwasilisha tatizo lako kwa maneno ya mdomo au katika maandishi kwa Mkurugenzi wa Kitengo cha Vijana na Familia Jiji la Salt Lake. Mkurugenzi wa Kitengo atajadili tatizo hilo na wewe na wafanyakazi wanaohusika kupata suluhisho.

Ikiwa tatizo lako halijasuluhishwa kukuridhisha, au kama una tatizo kumhusu Mkurugenzi wa Kitengo, unaweza kuweka matatizo yako katika maandishi kwa Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Jamii na Vitongoji Jiji la Salt Lake. Naibu Mkurugenzi atafanya uamuzi wa mwisho kuhusu jinsi suala hilo litakavyosuluhishwa na kutuma barua pepe kwa mshiriki.

## SHERIA ZA PROGRAMU YA YOUTHCITY NA MPANGO WA USIMAMIZI WA TABIA

Tunaamini washiriki wawe na burudani sana huku wakijiheshimu wenyewe, wakiwaheshimu wengine na wakiheshimu mazingira ya YouthCity. Ili kuwezesha mazingira salama na ya kusitawisha ya kujifunza tuna sheria 3 rahisi:

### 1. JIHESHIMU MWENYEWE

- Shiriki katika madarasa na programu za YouthCity
- Kuonesha tabia njema na kuwa mpole
- Kuongea na kutenda ifaavyo muda wote. Hii inamaanisha hakuna lugha mbaya (kutukana) kwa maandishi au kwa kuongea
- Uje umejiandaa kwa ajili ya shughuli na madarasa ili uweze kushiriki kikamilifu
- Kuongea na mtu mzima papo hapo ikiwa unahisi umeonewa

### 2. HESHIMU WENGINE

- Fuata maelekezo mara ya KWANZA yanapotolewa–wafanyakazi wapo kukusaidia uwe salama na uburudike
- Chunga mikono, miguu, na vitu vyako vyote. YouthCity haivumilii KABISA vurugu
- Baki katika sehemu ya jengo la YouthCity muda wote
- Kuwa pamoja – baki ndani ya upeo wa kuona wa wafanyakazi wa YouthCity muda wote
- Fuata kanuni kuu–watendee wengine namna unavyotaka kutendewa
- Sema “Samahani” inapohitajika
- Jitoe kusaidia wengine
- Epuka kuja na pesa na kununua vitu kutoka kwa wachuuzi wa vyakula na mashine sarafu za kuuzia bidhaa ndogo ndogo
- Ongea na mtu mzima papo hapo ikiwa unaona uonevu

### 3. HESHIMU MAZINGIRA

- Kuwa mwangalifu na mali, vifaa, na kompyuta zote za YouthCity
- Weka vitu mbali kadri unavyokwenda hakikisha kila sehemu ni safi zaidi kuliko ulivyoikuta
- Tembea kwa ukimya pindi uwapo ndani ya majengo
- Kuwa na heshima pindi unaposafiri katika gari la YouthCity
- Mikanda ya siti ni lazima ifungwe muda wote
- Chunga mikono yako
- Punguza sauti yako
- Baki kwenye kiti yako
- Furahia kula na kunywa tu pindi ukipewa ruhusa na wafanyakazi wa YouthCity
- Acha vitu vya kuchezea/michezo/vitu vya umeme maana vitavuruga programu na madarasa yetu

## SHERIA ZA PROGRAMU YA YOUTHCITY NA MPANGO WA USIMAMIZI WA TABIA INAENDELEA

| TAHADHARI | ONYO | UTULIZAJI | MATOKEO |
|---|---|---|---|
| Wafanyakazi wa YouthCity watampa mtoto TAHADHARI pindi anavyoonesha hisia, tabia au uchaguzi wake haufai kwa mazingira husika. TAHADHARI inatolewa kuwafahamisha vijana kwamba kile wanachofanya sio sawa na wafanyakazi watatoa maelekezo na/au kuwaelekeza tena ili vijana waweze kufanya chaguo tofauti wanavyokwenda mbele.<br><br>Wafanyakazi wanatumia TAHADHARI kusaidia kufahamisha na kufundisha tabia yenye heshima na ya kufaa kwa YouthCity. Wafanyakazi huwasaidia vijana kufikiria machaguo yao na kujiwajibisha binafsi kwa ajili ya machaguo yao. | Wafanyakazi wa YouthCity watatoa ONYO pindi hisia au tabia isiyofaa na/au chaguo duni likiendelea. ONYO linatolewa kama kuelekeza tena na ukumbusho thabiti wa ni nini kinatarajiwa YouthCity.<br><br>Wafanyakazi hutumia MAONYO kuwafundisha vijana ni tabia gani inatarajiwa YouthCity na kuimarisha mbinu za kujirekebisha mwenyewe. Wafanyakazi huwasaidia vijana kufikiria machaguo yao na kujiwajibisha binafsi kwa ajili ya machaguo yao. | Wafanyakazi wa YouthCity watatekeleza UTULIZAJI pindi kijana asipoheshimu mazingira husika, washiriki wengine, au yeye mwenyewe. UTULIZAJI unatumika ikiwa tabia au majibu mabaya yanaendelea kuongezeka. Pindi kijana AKITULIZWA anaondolewa kwa kipindi kifupi kwenye shughuli na anakaribishwa kutulia, kupata udhibiti na kufikiria tena machaguo yake.<br><br>Wafanyakazi watatekeleza UTULIZAJI kumfundisha kijana kwamba kujipa nafasi na kuzuia mienendo hasi ya tabia ni msingi wa kukuza udhibiti binafsi. Baada ya kijana kupata udhibiti na kuweza kujiwajibisha kwa tabia na machaguo yake anaweza kurudi kwenye shughuli au kundi husika. Wafanyakazi watamsaidia kijana kufikiria matendo yake na kujiwajibisha binafsi kwa ajili ya machaguo yake. | Uongozi wa Programu ya YouthCity utatoa MATOKEO kutokana na tabia hasi inayoendelea na / au inayoongezeka. MATOKEO yanaweza kuhusisha kuondolewa kwa muda mfupi kutoka kwenye shughuli husika, shughuli mbadala, kusimamishwa, au kufukuzwa kutoka kwenye programu. Uongozi wa programu utawataarifu wazazi kadri inavyohitajika.<br><br>Wafanyakazi hutumia MATOKEO kuwasaidia vijana kujiwajibisha kwa ajili ya machaguo, majibu, na tabia zao. |

**UGOMVI WA KIMWILI / KUKOSA UVUMILIVU KABISA:**

Ni wajibu wetu kuwaweka watoto na wafanyakazi wote katika usalama. Ili kusaidia kuhakikisha usalama, mtoto yote anayejihusisha katika mzozo wenye ugomvi wa kimwili atasimamishwa.

**KUSIMAMISHWA na KUFUKUZWA:**

Ikiwa tabia hasi itaendelea, inawezekana mshiriki akasimamishwa na/au kuondolewa katika programu. Kabla ya mtoto aliyesimamishwa kustahiki kurudi YouthCity, mshiriki wa programu, mzazi/mlezi na Msimamizi wa Programu wa Kijamii ni lazima wahudhurie kikao kujadili matarajio ya tabia ya baadaye na uwezekano wa kurudi kwenye ushiriki kamili katika programu za YouthCity.

---

SAINI YA MSHIRIKI: ______________________ TAREHE: ___/___/______
siku/mwezi/mwaka

SAINI YA MZAZI: ______________________ TAREHE: ___/___/______
siku/mwezi/mwaka